

نصيحة قصيرة للأباء والشباب

-لجمعنا البراءة - الذين يعيشون

في أوروبا

**Nasiha Chihaba Ya Wazazi Na Wabjana
Mujtama'a Yiitru Ya Wantru Wa Miini
Hukalranto Urupa**

كتبه: الشيخ محمد خليفة البراوي

**تحرير نجيب عبد القادر عمر بن شداد
وعبد الرحمن قلتين**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Nukhta ya Kaandha:

Alhamdulillah, umuhimu ya wazaazi khsherekela karka tarbiya ya wana waawo, wondiwo wa kaandha huwapo Tarbiya ya wanawawo, na mas'uliya upanza iluyawo ni muhimu zaidi karka diini yiit ya islamu, haqiqiqa mawducu ya tarbia, na qtilo Waqt naq powa ihtimamu wabjana na jili ya mustaqbali, ni muhimu zaidi ilu ya wazazi na wazeele, na hadafu nkulu ni kokdowa thuriya na mullo, na kuwa wakula qkoda waana karka ndila sura, kuwa wantu weema, na kubarata diiniyawo na duniya yawo, na kuwa waana masa'iidi karka daarayni duniya na akhera, kuwa wantu masalihi wenye taqwa na imaani na tawhiidi khalisi.

Allah (SWT) Bayiniile karka Qur'an hadiile:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا قُوَا أَنفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا﴾

[Ewe wantu weema, Mumini, badbadishani nafsi ziinu na ahli yiinu Mullo]

(قَالَ عَلَيْيُ بْنُ أَيِّ طَالِبٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ: عَلِمُوهُمْ وَأَدْبُوهُمْ).

Sayyidinaa Ali ibn Abi Taalib hadiile: "Wabarsheeni Diini na wa Adabisheeni".

(وَمَعْنَى: قُوَا أَنفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ) بِالرَّتِيْبَةِ وَالْتَّعْلِيْمِ وَالْتَّأْدِيْبِ.

Ni kubarshowa adabu, na Tarbiya, na ilmu.

Takiwa kuwa mas'uuliya iyi ni nkula na ni khatari, kaqisa muntu halawili na taqpatikano khalal kaake, iwa kuwa uquubaye ni Mulo.

Allah fanyize Du'a ya wazazi karka du'a ya wantu weema, hudu'iloo wanawawo.

Allah (SWT) hadiile:

﴿وَالَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ أَرْوَاحِنَا وَدُرِّيَاتِنَا فُرْةً أَعْيُنٍ وَاجْعَلْنَا لِلنُّمَّقِينَ إِمَامًا﴾

[Wantu weema] ni awaje huhado [karka du'a yawo] Mooja chi hebele karka wake wiitu, na thuriyya yiit, (wafanye) raaha ya maato, hubardisho maato, na shfanye Ma imamu, karka wenye taqwa. (Wa ongozi karka wantu). Waqtii ya wazaazi huwono wana wawo, kuwa wo ni weema, karka taqwa, na masalihi, ntaku shaka kuwaawo watakuwa Raaha na bardi ya Maato yawo, Na Mtrume (ﷺ) hadiile:

(كُلُّكُمْ رَاعٍ وَكُلُّكُمْ مَسْئُولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ).

“Wotte wiinu ni Maloojiri, npeela Mas’uliya, na wotte wiinu ntaysu’ala toowa Mas’uliya yani rashiliiza”.

Na karka hadiithi yiingine Mtrume (ﷺ) hadiile:

(كَفَىٰ بِالْمَرءِ إِثْمًا أَنْ يُضَيِّعَ مَنْ يَعْوُلُ أَوْ يَقْوُتُ). رواه أبو داود.

“Humtosheleza madambi muntu kuwaye naku dayi’a/waqpoteza mas’uliya ya ahliye”.

Nukhta ya Piili:

1: Nasiiha ya kaandha: kubarata ilmu khaasa ilmu Aqiida, ndiyo itamdhoro na itamtilo Amaniini na uDhalala, na fikrah mbovu.

2: Ya piili: Kuwaye nakufanya weenza muntu wasura, muntu meema.

Mtrume (ﷺ) hadiile:

(لَا تُصَاحِبْ إِلَّا مُؤْمِنًا).

“Sim fanye meenza ila mumini”.

3: Mubjana kuwaye kumeera raadhi ya Mujiitru na qtuluba qpata kookolowa na mulo. Qfanya zeema, na keepuka ziwovu.

4: Ku hafida huduudi ya Mujiitru, Mujiitru taku nafidho: Mtrume (ﷺ) hadiile:

(احْفَظِ اللَّهَ يَحْفَظُكَ).

“mhafidhe Allah, huduudi ya Mujiithu naye naku hafidha”.

Keepuka madambi, na macaasi.

5: Nasiiha ya wabjana, ni qtaala nasiixa ya mithume ya wantu weema. Qshiika Towhiidi ka mikono miwiliye na migoyiini.

Nukhta ya thaathu:

Hiskitishe zaydi kuwona wabjana wiit wa Miini kiingila jawabu za gang, na dorogo. Wabjana wiingi wako karka ndila sura maisha masura, siwo magang, wala siwo waamo

karka rabsha, na karka crime. Walakini waako numbari haba ya wabjana ingilo karka grubo izo za gangs. Why ama kaqisani yaawo wa ingiilo.

1. Wako bacdhii ya wabjana humera safety qapata amaan kuwaye umo karka grup ya weenza naawo ni ma gang. Lakini ye umo qapata amanii
2. Wako wiingine hapendi masoomu, kaqisa ye siwo barabara na masoomu hapendi skoola
3. Wako wiingine wanayo, family problems. Maama na baaba walateene karka numba ntayo mubli waaye humtiyo, hufanya yaaye nasuulo
4. Na wabjana wiingine hiingila 4 gang kaqisa weenzawe ndiwo ma gang ama wantu wakuluwe wa tilo tilo.

Isa halli niyo?

1. Hali mzeelo husulowa qkoda na manawe
2. Mkase problema yaye nayo
3. Meera hufanyani, weenzawe ni naani
4. Mzeelo husulowa qsima qtala mas'uliya kuwa na maanawe, koda naye, msayde mfanye meenza. Dadaalata kumeerela masoomu, ku badila maishaye.

Nukhta ya Nne:

Umuhiimu wa Tawhidi na Aqiida ya muntu mislamu nawe mkulu ama chihaba ni muhimu zaydi:

1. Tawhiidi na Aqiida ni Asaasi ya Diini na kila ibaada ama mu'amalati na tabia yote iwashila ka Aqiida na Tawhidi. Tawhiidi ni kama nguzo na Asaasi ya Numba na mi nkutta na chidanka ni ibaada na mu'amalati, na tabia muntu ntana Tawhidi ntana Asaasi ya Diini na Ibaada yake haitaqabalowi na iteyiwi sahihiha.
2. Aqiida na Tawhiidi ni chintu cha kandha muntu humingizo karka Diini kalima ya Shahada لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ ntaku ilaahi ya haqi ila Allah, na Muhammad ni Mtrume wa Mujiitru, hal maza muntu iwiilo kuwa Tawhiidi ni Muhimu husulowa kuwaye, kuwaye na kuluta si raashe Ahkaamu zaake.
3. Ntaku muntu takingilo Amanini Sku ya Qiyama ila ka Tawhidi na Aqiida khalisi Mujiitru (SWT) hadiile:

يَوْمَ لَا يَنْفَعُ مَالٌ وَلَا بَنْوَنٌ إِلَّا مَنْ أَنْقَلَهُ اللَّهُ بِقُلْبٍ سَلِيمٍ ﴿١﴾

“Munti hayiinfii Maali wala Waana, ila Muntu takuuyo na Qalbi saliimu”.

4. Tawhiidi na Aqiida ni moyi karka asbaabu muntu hum hafido na adkaari mbovu na ihdadi ku inkiroowa Mujiitru, na udalaala.
5. Tawhiidi na Aqiida saafi, sahiha muntu hum dhoora qpotela karka shirki, na shirki ni dambul akbari. Muntu chifa ka shirki takingila muloni, na Mujiitru hum gafirile ma dambize.

Kubarata Tawhiidi tambarata mooja, takubarata maina yaake na sifa zaake.

Nukhta ya Taano:

Ichiwa we naqpenzeleza darsi qtomolowa yes yiiko, audio ama video Tafsiiri Juz Ama Tabaraka, na ziwo za Tawhiid nsomele Uthuulu Thalatha, Qawaad arba'a hatu kitaab Tawhiidi. Na'isa kusomesha online kila jimatatu na arabiya Qur'ani, Tajwiidi na Fiqhi. Ama ichiwa we naqpenzeleza Tafsiiri ya Mandishi Ntaasa skuwona, Tafsiiri ya Chimiini ama ziwo za Tawhiidi ka Chimini in sha Allah fil mustaqbal chinayo niyyah qfanya tafsiiri ka chimini na qfasira ziwo la Tawhidi.

Nukhta ya sita:

Yes, yiiko fursa bal fursa niingi ichiwa wako wabjana wanayo intresta wanaq suulo keenda itaqa diroowa bal wako wabjana wa Miini enzelo Jama'a Madiina hukalanto UK. Qariibku muliza, basi ichiwa wako wabjana wanasulo. Kendha chiko tarayi kuwa sayda chinayo wantu taku wasaydo in sha Allah.